## Maswali

1. Musa alijifunza nini alipokuwa akiishi na wazazi wake?
2. Musa alienda kukaa wapi alipokuwa mkubwa?
3. Mbona Musa alitoroka?
4. Alienda kukaa wapi?
5. Musa aliishi na nani?
6. Musa alifanya kazi gani alipokuwa kwa nchi ya Midiani?
7. Musa aliona kitu gani cha maajabu karibu na Mlima wa Horebu?
8. Mungu alimwambia Musa afanye nini?
9. Mungu alimpa Musa ishara mbili gani?
10. Mungu alituma nani asaidie Musa?

## Majibu

1. Musa alijifunza kupenda na kutii Mungu.
2. Musa alienda kukaa kwa nyumba ya kifalme na binti wa Farao.
3. Musa aliua Mmisri aliyekuwa akimpiga Mwisraeli. Farao alijua na akataka kumua Musa. Musa aliogopa.
4. Musa alienda kukaa kwa nchi ya Midiani.
5. Musa aliishi na Yethro na familia yake.
6. Musa alichunga mifugo ya Yethro.
7. Musa aliona kichaka kikichomeka, lakini hakikuungua.
8. Mungu alimwambia Musa aongoze Waisraeli kutoka Misri, waende kwa nchi ya Kanaani.Mungu alimwambia Musa amwambie Farao awaache waende.
9. Fimbo ya Musa iligeuka ikawa nyoka. Mkono wa Musa uligeuka ukawa nyeupe na ukoma.
10. Mungu alituma Haruni asaidie Musa.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 2    Mwaka wa 1

# 17 Musa aona kichaka kikichomeka

**Kwa Biblia** Kutoka 2:11-25; Kutoka 3; Kutoka 4: 1-17

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu ni mkuu sana. Lazima tumtii kabisa. Mungu hutusaidia kufanya haki.

### Somo

Musa alipokuwa mdogo alikaa na mama na baba yake. Walimfunza juu ya Mungu. Walimwambia vile Mungu alilinda Nuhu, Ibrahimu, Isaka, Yakobo, na Yusufu. Walimwambia juu ya ahadi alizoahidi watu wake. Musa alikua akipenda na kumwamini Mungu. Musa aliona vile wazazi wake waliumia kama watumwa wa Wamisri. Alitamani Mungu awasaidie.

Musa alipokua mkuwa, alienda kuishi kwa nyumba ya kifalme. Binti wa Farao aliyemuokota kwa manyasi ndiye alikuwa ‘mamaye’ mpya. Musa alikuwa na nguo nzuri na maisha ya furaha kwa nyumba ya kifalme. Lakini hakusahau familia yake ya kweli.

Siku moja, Musa alipokua mkubwa, aliona Mmisri akimpiga Mwisraeli mtumwa. Musa alikasirika sana. Hakupenda kuona watu wakifanyiwa ukatili. Ukweli Musa alikuwa Mwisraeli, ingawaje aliishi kama Mmisri kwa nyumba ya kifalme. Musa alikasirika sana akumpiga Mmsri na kumua. Musa alipoona alicho- kitendo aliogopa. Alizika Mmisri mchangani na kutoroka. Lakini mtu alikuwa amemuona Musa akiua Mmisri. Farao aliposikia, alitaka kumwua Musa. Musa alitoroka na akaenda nchi ya mbali. Alitoroka na kuenda nchi ya Midiani.

Safari ya kuenda Midiani ilikuwa ndefu. Musa alichoka na kuwa na kiu kwa ajili ya safari hiyo ndefu. Alifika kwenye kisima na akakaa chini ili anywe maji na kupumzika. Kulitokea wanawake waliokuja kupea mifugo ya baba yao maji. Wale wanawake walipofika kisimani, kulikua na wachungaji walioteremka kutoka kilimani na kuwafukuza. Musa alikasirika. Aliwafukuza wale wachungaji. Halafu akawasaidia wale wanawake kupea mifugo yao maji.

Wale wanawake na Yethro baba yao walishukuru Musa kwa huo usaidizi. Walikaribisha Musa kukaa nao. Musa alikaa kwa Yethro. Alimchungia mifugo kwa miaka mingi. Alioa Sipora bintiye Yethro. Walipata wana wawili. Wakati huo wote Waisraeli walipokuwa Misri waliomba Mungu. Waliomba Mungu awaokoe kutoka kwa Wamisri waliokuwa katili sana. Mungu alisikia maombi ya Waisraeli. Mungu alikuwa tayari kuwaokoa. Mungu alikuwa amechagua Musa kufanya hii kazi kubwa. Alikuwa amechagua Musa kuwatoa Waisraeli Misri na kuwaongoza mpaka nchi yao.


Mungu alitumia maisha ya Musa kufanya kazi yake. Kwanza Musa alilelewa na mamaye Mwisraeli. Alijifunza kupenda Mungu na watu wake Waisraeli. Baadaye alikaa miaka mingi kwa nyumba ya kifalme. Alikuwa mwana wa mfalme Mmisri. Alijifunza kuwa askari tena mtawala. Lakini alitakiwa awe mvumilivu na mpole. Alitakiwa ajifunze kuamini Mungu sio mwenyewe. Alijifunza hii alipokuwa mchungaji kwa nchi ya Midiani. Kwa hivyo Musa alikuwa tayari kwa kazi Mungu alimchagua afanye.



Siku moja Musa alipeleka kondoo mbali kutafuta nyasi. Alienda mwisho wa changwa karibu na Mlima wa Horebu. Musa aliona maajabu. Kando ya kilima kichaka kilikuwa kinachomeka. Kichaka kilichomeka, kikachomeka, lakini hakikuungua. Musa alienda kuangalia huo moto wa kimaajabu.

Musa alipokua akija karibu na kichaka, malaika alimwita, “Musa! Musa!” Malaika alimwambia Musa kutoa viatu kwa sababu alikuwa amesimama mahali patakatifu. Mungu alimwambia kwamba alikuwa amesikia maombi ya Waisraeli huko Misri. Alikuwa anaenda kuokoa Waisraeli kutoka kwa Farao. Mungu alimwambia kwamba alikuwa amemchagua yeye Musa kuongoza Waisraeli kwenda nchi ya Kanaani kupitia jangwani. Mungu alimwambia aende Misri na aulize Farao aachilie Waisraeli waende.

Musa aliona hataweza hiyo kazi kubwa. Mungu alimwaahidi Musa kwamba atakuwa naye. Kwamba atamsaidia. Mungu alimwambia Musa jina lake, “MIMI NDIMI NDIYE”



Mungu alimpa Musa ishara mbili za kuonyesha Waisraeli na Farao. Ishara zitaonyesha kwamba ametumwa na Mungu. Musa alikuwa na fimbo mkononi. Mungu alimwambia aitupe chini. Musa alipoitupa chini, iligeuka kuwa nyoka na kuanza kutelezateleza sakafuni. Musa alipoichukua iligeuka kuwa fimbo tena.

Mungu alimwambia Musa kuweka mkono ndani ya koti. Musa alipoitoa nje, mkono wake ulikuwa nyeupe na ugonjwa wa ukoma. Musa alirudisha mkono ndani ya koti. Alipoitoa nje ilikuwa sawa.

Musa alikuwa bado na shaka juu ya kazi aliyopewa na Mungu kufanya. Mungu alituma Haruni nduguye  amsaidie. Musa na Haruni walirudi Misri. Walionyesha Waisraeli ishara za Mungu. Waisraeli walifurahi sana kuona kwamba Mungu atawaokoa na kuwatoa utumwani Misri.

Musa na Haruni walienda kuuliza Farao aachilie Waisraeli waende. Farao alikasirika na kusema, “Bwana ni nani, ndio nimtii. Sitawaacha watu waende.” Farao alikasirika sana na akawaongezea kazi. Farao aliumia sana alipokataa kutii Mungu. Baada ya mda, Farao alikubali kwamba yote yalifanyika kwa uwezo wa Mungu. Mwishowe alikubali na akawaacha Waisraeli waende.